



do 1 thing

Misheni ya Do 1 Thing ni kuwahimiza watu, familia, biashara na jamii kujiandaa kwa hatari zote na kuweza kukwepa msiba.

LENGO: Kuwa na maji ya kutosha mkononi kwa ajili ya familia yako inayoweza kudumu siku 3 (saa 72). Hii inapaswa kuwa karibu galoni 3 kila mtu.

Maji

Iwe unapata maji kutoka kwa mfumo wa maji wa manispaa au nyumba yako ina kisima cha kibinafsi, maji yako yanategemea kuwa na uwezo wa kutumia mfumo. Wakati wa kupotea kwa umeme huenda ukajipata bila maji ya kunjwa. Huenda pia ukahitaji maji ya dharura ya kunywa kama maji yako yamechafuka. Visima vya kibinafsi na mfumo wa maji ya manispaa vinaweza kuathiriwa na uchafu wakati wa msiba.

Chagua moja kati ya mambo yafuatayo ya kufanya mwezi huu ili ujiandae vyema:

- Nunua na uhifadhi maji ya chupa yanayouzwa yanayoweza kudumu saa 72 (au zaidi - hadi wiki mbili).**

Maji ya siku tatu kwa mtu mmoja ni galoni 3 ya maji (galoni moja kwa kila mtu kwa siku). Jumuisha pia galoni moja ya ziada kwa mnyama kipenzi wa wastani. Galoni hiyo moja inapaswa kudumu siku tatu, lakini panga kwa zaidi kau chache ama mnyama wako kipenzi ni mkubwa au ni mdogo zaidi.

Siku 1, mtu 1 - galoni 1 (au aushi 128) = 7 - chupa za aushi 20 = lita 4
Siku 3, mtu 1 - galoni 3 (au aushi 384) = 21 - chupa za aushi 20 = lita 12

Wakati wa dharura, unapaswa kunywa angalau kwati mbili (galoni moja nusu) ya maji kwa siku. Kunywa kwati 3-4 kwa siku kama uko katika eneo lenye joto, mjamzito, mgongjwa au ni mtoto. Maji mengine katika maji yako ya dharura yatatumiwa kwa kupika au usafishaji.

Ukinunua maji yanayouzwa ya chupa, yanapaswa kubadilishwa mara moja kwa mwaka. Hifadhi maji yako katika mahali baridi, penye giza ili yawe safi kwa muda mrefu.



Maji yakipungua, usigawe maji. Kunywa kiwango unachohitaji leo na utafuta zaidi kesho.

Hifadhi maji ya saa 72 nyumbani.

Ukipata maji yako kutoka kwa kisima cha kibinafsi, safisha maji yako ya mfereji kabla ya kuyahifadhi. Weka matone sita ya pausha kwa galoni ya maji, tikitisa vizuri, kisha wacha yatulie kwa dakika 30. Ukipata maji yako kutoka kwa mfumo wa maji wa manispaa, hakuna hitaji la kusafisha maji ya mfereji kabla ya kuyahifadhi.

Badilisha maji yako kila miezi sita kama unahifadhi maji yako mwenyewe. Daima safisha chupa kabla ya kuzijaza. Hifadhi maji yako katika mahali penye baridi na giza.

Safisha chupa kabla ya kujaza:

- (1) Safisha kontena na sabuni na usuze na maji
- (2) Safisha kwa kuosha na mchanganyiko wa kijiko 1 cha pausha ya klorini kwa kwati ya maji kwenye maeneo yote ya ndani ya kontena.
- (3) Ruhusu hewa ikaushe kwa angalau dakika moja

Tumia chupa wazi za plastiki na vifuniko vinavyofunga kabisa. Jagi za maziwa hazina kontena nzuri za kuhifadhi maji, hazifuniki vizuri, na maji yaliyohifadhiwa ndani yake yanaweza kukuza uchafu wa plastiki. Tumia tu chupa ambazo kimsingi zilikuwa na vinywaji ndani (plastiki kubwa za chupa za soda hufanya kazi vizuri). *Ona ukurasa wa awali ili kung'amua kiwango cha maji unapaswa kuwa nacho cha familia yako wakati wa dharura.*

Jifunze jinsi ya kutoa maji salama ya kunywa ya kaya yako wakati wa msiba.

Kichemsha Maji - USITUMIE kama tangi au mapambo yamezama katika maji ya mafuriko!

- (1) Zima gesi au umeme unaoingia kwenye kichemsha maji (zima umeme katika kisanduku cha fusi au cha mzunguko, zima gesi kwa kutafuta valvu inayotoa kichemshaji cha maji moto na kuzima kishika valvu ili ipindane - haijalinganishwa na - mstari wa gesi)
- (2) Zima valvu ya kuingiza maji (inapaswa kuwa karibu na kichemsha maji)
- (3) Fungua kitoa maji chini ya tangi
- (4) Washa mfereji wa maji moto (maji itatoka kutoka kwa tangi, sio kwenye mfereji)

Tupa galoni chache za kwanza kama zina mabaki ya kutu. Usiwashe gesi au umeme hadi tangi ijae upya.

Mabomba

- (1) Zima valvu kuu ya maji ambapo maji yanaingia katika nyumba (kwa kawaida karibu na mita ya maji kama una maji ya mji).
- (2) Ruhusu hewa kuingia kwenye mabomba kwa kuwasha mfereji wa juu zaidi katika nyumba yako.
- (3) Pata maji kutoka kwa mfereji wa chini kabisa katika nyumba yako (usipate kamwe maji kutoka kwa mifereji ambayo imeingia katika maji ya mafuriko).

Barafu - Kama una nafasi ya friza, zingatia kugandisha sehemu ya maji yako. Hii ina faida zaidi ya kuweka chakula katika friza barida kwa muda mrefu zaidi wakati umeme umepotea.